TANGAZO LA SERIKALI Na. 260 la tarehe 25/4/2025

SHERIA YA MADINI,
(SURA YA 123)

# KANUNI

(*Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 129)*

KANUNI ZA MSAADA WA KIUFUNDI KWA WAMILIKI WA LESENI NDOGO ZA UCHIMBAJI MADINI ZA MWAKA 2025

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*


SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
UTOAJI WA MSAADA WA KIUFUNDI KWA WAMILIKI WA LESENI NDOGO ZA UCHIMBAJI MADINI

4. Msaada wa kiufundi.
5. Idadi ya leseni za msaada wa kiufundi.
6. Wajibu wa afisa madini mkazi.
7. Wajibu wa mwezeshaji.
8. Wajibu wa mmiliki wa leseni.
9. Mgawanyo wa faida ya uwekezaji.
10. Usimamizi wa mgodi.
11. Uingizaji wa vifaa na mitambo.
12. Usalama na ulinzi wa eneo la leseni.
13. Muda wa mkataba.
14. Usajili wa mkataba.
15. Kurekebisha mkataba.

16. Kuvunja mkataba.
17. Lugha ya mkataba.
18. Notisi.
19. Sheria inayosimamia mkataba.
20. Utatuzi wa mgogoro

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YA JUMLA

21. Usimamizi na ufuatiliaji wa mikataba.
22. Ukiukwaji.

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

JEDWALI

SHERIA YA MADINI,
(SURA YA 123)

## KANUNI

(*Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 129)*

KANUNI ZA MSAADA WA KIUFUNDI KWA WAMILIKI WA LESENI NDOGO ZA UCHIMBAJI MADINI ZA MWAKA 2025

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Msaada wa Kiufundi kwa Wamiliki wa Leseni Ndogo za Uchimbaji Madini za Mwaka 2025.

Matumizi

**2.** Kanuni hizi zitatumika kwa wamiliki wa leseni ndogo za uchimbaji madini.

Tafsiri

**3.** Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"afisa madini mkazi" maana yake ni afisa madini mkazi aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 27 cha Sheria;

"Katibu Mtendaji" maana yake ni Katibu Mtendaji aliyeteuliwa kwa mujibu wa Sheria;

"mkataba" maana yake ni mkataba wa msaada wa kiufundi utakaoingiwa kati ya mmiliki wa leseni na mwezeshaji;

"mmiliki wa leseni" maana yake ni mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji madini;

"msaada wa kiufundi" maana yake ni utaalamu wa uchimbaji, mitambo au mashine mbalimbali, namna ya uendeshaji wa mitambo, au ujuzi wa kufanya shughuli za madini usiopatikana nchini Tanzania, unaotolewa kwa lengo la kusaidia utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, ujuzi wa madini yanayokusudiwa kuchimbwa katika leseni ya uchimbaji mdogo kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 8(3) cha Sheria;

"mwezeshaji" maana yake ni mtu, kikundi cha watu au kampuni inayotoa msaada wa kiufundi kwa mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji madini kwa mujibu wa kifungu cha 8(3) cha Sheria;

Sura ya 123

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Madini;

"Tume" maana yake ni Tume ya Madini iliyoanzishwa chini ya Sheria; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya madini.

## SEHEMU YA PILI
## UTOAJI WA MSAADA WA KIUFUNDI KWA WAMILIKI WA LESENI NDOGO ZA UCHIMBAJI MADINI

Msaada wa kiufundi

**4.** Mmiliki wa leseni atapatiwa msaada wa kiufundi kupitia mkataba wa maandishi utakaoingiwa kati yake na mwezeshaji.

Idadi ya leseni za msaada wa kiufundi

**5.** Mmiliki wa leseni atakuwa na haki ya kuingia mkataba wa kiufundi na mwezeshaji mmoja kwa leseni ndogo za uchimbaji madini zisizozidi kumi kwa mkataba mmoja, kwenye eneo moja.

Wajibu wa afisa madini mkazi

**6.**-(1) Afisa madini mkazi atakuwa na wajibu wa-.

(a) kukagua leseni inayoombewa msaada wa kiufundi;

(b) kubaini shughuli za uchimbaji madini zinazoendelea katika leseni na iwapo kuna migogoro yoyote;

(c) kuhakiki iwapo mmiliki wa leseni ana madeni ya leseni au hati ya makosa katika ofisi nyingine za madini;

(d) kubaini iwapo kuna migogoro yoyote ya kisheria, kiuendeshaji, au kikatiba inayohusu ombi husika iwapo leseni inamilikiwa na kikundi au kampuni; na

(e) kuwasilisha kwa Katibu Mtendaji taarifa ya ukaguzi yenye ushauri na mapendekezo iwapo mmiliki wa leseni anastahili au hastahili kupata msaada wa kiufundi.

(2) Taarifa itakayoandaliwa katika kanuni ndogo ya (1) itajumuisha taarifa zilizoainishwa katika Jedwali.

Wajibu wa mwezeshaji

**7.-**(1) Mwezeshaji atakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kutoa msaada wa kiufundi kuhusu utafutaji wa madini, uchimbaji, mitambo, mashine mbalimbali, na utaalamu au ujuzi wa shughuli za madini na uchenjuaji wa madini;

(b) kuhakikisha miundombinu yote isiyohamishika inazingatia kanuni na taratibu za utunzaji mazingira;

(c) kuhakikisha kuwa vifaa anavyovitoa kwa mmiliki wa leseni vinakuwa sehemu ya mkataba na iwapo mkataba utakoma kutokana na sababu mbalimbali zilizobainishwa, mwezeshaji atakabidhi kwa mmiliki wa leseni vifaa vya utafiti, uchimbaji na uchenjuaji kama ilivyokubaliwa kwenye mkataba;

TS. Na. 305 la 2018

(d) kwa kushauriana na mmiliki wa leseni, ataandaa mpango madhubuti wa urithishaji maarifa, ujuzi, utaalamu na matumizi ya teknolojia kwa watendaji wa mmiliki wa leseni kwa kuzingatia mahitaji kama ilivyobainishwa katika Mwongozo wa Tume wa Uwasilishaji wa Mpango wa Ushirikishwaji wa Wazawa kwenye Shughuli za Madini;

(e) kwa kushirikiana na mmiliki wa leseni, kuandaa mpango madhubuti wa miradi ya wajibu wa wamiliki wa leseni kwa jamii;

(f) kufanya utafiti katika eneo la leseni husika wakati uchimbaji wa madini unaendelea;

Sura ya 191

(g) kuwasilisha mpango wa athari za kimazingira ulioidhinishwa na mamlaka husika kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira kabla au ndani ya siku mia moja na ishirini baada ya kupata ridhaa ya Tume ya kuanza uchimbaji katika eneo la leseni;

(h) kwa kushirikiana na mmiliki wa leseni, ataandaa mpango wa uchimbaji mgodi ambao utaidhinishwa kabla au ndani ya siku tisini baada ya kupata ridhaa ya Tume ya kuanza uchimbaji;

TS. Na. 408 la 2010

(i) kuandaa mpango wa ufungaji mgodi na kuuwasilisha kwa mujibu wa utaratibu ulioainishwa kwenye Kanuni za Usalama Mahali pa Kazi, Afya na Utunzaji wa Mazingira;

(j) kuandaa mpango wa utaratibu wa kubadilishana maarifa na taarifa za msingi kuhusu teknolojia inayotumika kwenye uzalishaji na shughuli za utafiti wa madini.

(2) Mwezeshaji atakuwa na mwakilishi wa kudumu ambaye atahusika katika kutoa taarifa zote zinazohitajika katika mgodi pindi mamlaka husika itakapozihitaji.

(3) Mipango iliyoandaliwa katika kanuni ndogo ya (1) itawasilishwa kwa afisa madini mkazi kama ifuatavyo:

(a) kwa mipango iliyorejewa katika kanuni ndogo ya (1)(h), (i) na (j), itawasilishwa wakati wa maombi ya ridhaa au ndani ya siku tisini baada ya kupata ridhaa ya Tume ya kuanza kutoa msaada wa kiufundi; na

(b) kwa mpango uliorejewa katika kanuni ndogo ya (1)(g), utawasilishwa wakati wa maombi ya ridhaa au ndani ya siku mia moja na ishirini baada ya kupata ridhaa ya Tume ya kuanza kutoa msaada wa kiufundi.

(4) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1)(c), iwapo sababu za ukomo wa mkataba zinatokana na makusudi au uzembe wa mmiliki wa leseni kwa kutotimiza wajibu wake katika mkataba, na kwa kuzingatia masharti ya mkataba, mwezeshaji anaweza kuondoka na vifaa vyake ikiwa yeye hajasababisha au hajahusika moja kwa moja na vitendo vilivyosababisha kuvunjika kwa mkataba huo.

Wajibu wa mmiliki wa leseni

**8.-**(1) Mmiliki wa leseni atakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kuzingatia Sheria na kanuni kuhusiana na taratibu za umiliki wa leseni na wajibu wake;

(b) kutokuingia makubaliano na mtu mwingine kwa nia ya kutekeleza majukumu ya aina moja au yanayofanana kwa karibu na yale ambayo mwezeshaji anatakiwa kuyatimiza kwenye leseni husika katika kipindi cha uhai wa mkataba pasipo makubaliano na mwezeshaji;

(c) kushiriki moja kwa moja katika usimamizi, uratibu, na utekelezaji wa shughuli zote za utafiti, uchimbaji, na uchenjuaji madini ndani ya eneo la leseni;

(d) kuhakikisha shughuli zote za uchimbaji na uchenjuaji madini zinafanyika ndani ya eneo la leseni;

(e) kwa kushirikiana na mwezeshaji, kuandaa mpango madhubuti wa miradi ya wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii;

(f) kuhakikisha tozo, mrabaha na ada zote za Serikali zinazotokana na leseni zinalipwa kwa mujibu wa sheria;

(g) kuhakikisha kuwa shughuli za uchimbaji zinafanyika kwa kuzingatia mpango wa usimamizi na utunzaji wa mazingira ulioidhinishwa; na

(h) ikiwa ameruhusu mchimbaji au wachimbaji wengine kufanya shughuli za uchimbaji katika kitalu au vitalu mbalimbali ndani ya eneo la leseni, atalazimika kuwa na makubaliano ya maandishi na wamiliki wa vitalu hivyo yakibainisha haki na wajibu wao ikiwemo kufanya kazi kwa pamoja wakiwa na mwezeshaji au kulipwa fidia ili kusitisha kufanya shughuli katika vitalu husika na kumuacha mmiliki wa leseni aendelee kuchimba mwenyewe kwa msaada wa kiufundi kutoka kwa mwezeshaji.

(2) Mpango na makubaliano ya maandishi yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1)(e) na (h) mtawalia, yatawasilishwa kwa afisa madini mkazi wakati wa uwasilishaji wa maombi ya ridhaa ya msaada wa kiufundi.

Mgawanyo wa faida ya uwekezaji

**9.** Mkataba utakaoingiwa kati ya mwezeshaji na mmiliki wa leseni utazingatia masharti ya mgawanyo wa faida za mradi kwa utaratibu ufuatao:

(a) mmiliki wa leseni atapata mgawanyo wa faida ghafi ya uzalishaji wa madini na makinikia usiopungua asilimia thelathini baada ya mrabaha, ada ya ukaguzi na tozo zote za Serikali kulipwa

bila kujali gharama za uendeshaji wa mradi zilizoingiwa na mwezeshaji; na

(b) endapo mmiliki wa leseni na mwezeshaji wataamua kuunganisha leseni ambazo zimeombewa msaada wa kiufundi kwa lengo la kupata leseni ya kati ya uchimbaji madini, watakubaliana kuhamisha leseni hiyo kwenda kampuni ya mwezashaji au kuanzisha kampuni ya ubia ili waweze kumiliki leseni ya kati ya uchimbaji madini kwa pamoja na kukubaliana kuhusu utaratibu wa mgawanyo wa faida za mradi kupitia leseni hiyo.

Usimamizi wa mgodi

**10**.-(1) Usimamizi wa shughuli za mgodi utakuwa ni jukumu la pamoja kati ya mwezeshaji na mmiliki wa leseni.

(2) Mmiliki wa leseni atakuwa na dhamana ya kusimamia na kuhakikisha kuwa sheria, kanuni na taratibu zinazingatiwa.

(3) Wafanyakazi katika mgodi watakuwa raia wa Tanzania pekee isipokuwa katika masuala yanayohitaji msaada wa kiufundi kwa mujibu wa Kanuni hizi.

(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (3), raia wa kigeni ataruhusiwa kufanya kazi katika eneo la leseni ndogo ya uchimbaji madini baada ya kukidhi matakwa ya sheria zinazohusiana na ajira kwa raia wa kigeni, na kabla ya raia huyo wa kigeni kuruhusiwa kuanza kufanya kazi katika eneo la leseni husika, mmiliki wa leseni atapaswa kuomba ridhaa kwa Tume ili raia huyo aruhusiwe kufanya kazi.

Uingizaji wa vifaa na mitambo

**11**.-(1) Mwezeshaji kwa kushirikiana na mmiliki wa leseni atahakikisha kuwa vifaa na mitambo kwa ajili ya kutoa msaada wa kiufundi vinaingia katika eneo la mgodi na kutumika kwa ajili ya shughuli za uchimbaji madini zilizokusudiwa.

(2) Mara baada ya vifaa na mitambo kuingia katika eneo la leseni, mmiliki wa leseni atatakiwa kutoa taarifa kwa afisa madini mkazi wa eneo husika kuhusu uwepo wa vifaa na mitambo hiyo.

(3) Taarifa itakayotolewa na mmiliki wa leseni chini ya kifungu kidogo cha (2) itahusisha idadi na aina ya vifaa na mitambo.

Usalama na ulinzi wa eneo la leseni

**12.** Mmiliki wa leseni na mwezeshaji watakuwa na jukumu la kulinda usalama wa mali na eneo la leseni wakati wote wa mkataba.

Muda wa mkataba

**13.**-(1) Mkataba wa msaada wa kiufundi utakuwa wa kipindi kisichozidi miaka mitatu kuanzia tarehe ya kusajiliwa.

(2) Mmiliki wa leseni, miezi mitatu kabla ya mkataba kufika ukomo, anaweza kuwasilisha kwa Tume maombi ya kuhuisha mkataba.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), uhuishaji wa mkataba unaweza kufanyika kwa kipindi kisichozidi jumla ya miaka kumi na mbili na kwa kuzingatia uhai wa leseni.

Usajili wa mkataba

**14.**-(1) Mikataba ya msaada wa kiufundi itakayowasilishwa itahakikiwa na kusajiliwa na Tume.

(2) Iwapo Tume itaamua kutosajili kkataba husika, itamjulisha mtu aliyewasilisha maombi kuhusu uamuzi huo.

Kurekebisha mkataba

**15**.-(1) Mmiliki wa leseni na mwezeshaji kwa pamoja na kwa makubaliano ya maandishi wanaweza kurekebisha baadhi ya vifungu vya mkataba iwapo wataona inafaa.

(2) Iwapo kutakuwa na mabadiliko ya sheria au kanuni ambayo yataathiri utekelezaji wa sehemu ya mkataba au mkataba wote, mwezeshaji na mmiliki wa leseni watajadiliana na kuingia makubaliano mapya kurekebisha sehemu ya mkataba iliyoathiriwa au kuhuisha mkataba wote ili kuendana na mabadiliko yaliyotokea.

(3) Endapo yatagundulika madini mengine yenye thamani kiuchumi na mmiliki wa leseni akaomba kwa Tume kuongezewa madini hayo kwenye leseni yake na akakubaliwa, pande zote mbili za mkataba zitawajibika kufanya marekebisho kwenye mkataba wa awali au kuingia mkataba mpya na kuongeza mgawanyo wa faida za mradi kwa uwiano wataokubaliana.

(4) Marekebisho yoyote yanayokusudiwa kufanyika katika mkataba yatawasilishwa kwa Tume kwa ajili ya kuridhiwa na kusajiliwa.

Kuvunja mkataba

**16**. Kila upande utakuwa na haki ya kuvunja mkataba kwa kutoa notisi ya siku thelathini kutokana na sababu zifuatazo:

(a) endapo upande mmoja hautaridhishwa na utekelezaji wa masharti ya mkataba;

(b) kuisha kwa madini katika eneo la leseni linalohusika;

(c) endapo upande mmoja utabaini vitendo vya udanyanyifu kama vile wizi wa madini, mitambo, vifaa na mali nyinginezo zilizopo mgodini na udaganyifu kuhusu ukokotoaji wa kiwango cha madini kilichozalishwa, au udanganyifu wa aina nyingine utakaoathiri utekelezaji wa mkataba;

(d) endapo leseni itafutwa; na

(e) endapo leseni itafikia ukomo na kutohuishwa.

Lugha ya mkataba

**17**. Katika kuandaa mkataba wa msaada wa kiufundi, lugha ya mkataba itakuwa Kiswahili au Kiingereza.

Notisi

**18**. Taarifa zote zinazohusu utekelezaji wa mkataba zitawasilishwa kwa wahusika wa mkataba kwa njia ya barua pepe, kwa mkono, au anuani ya posta, au njia nyingine ambayo watakubaliana.

Sheria inayosimamia mkataba

**19**. Mkataba utakaoingiwa kati ya mmiliki wa leseni na mwezeshaji utatafsiriwa na utatekelezwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania.

Utatuzi wa mgogoro

**20**.-(1) Bila kuathiri masharti ya Sheria na Kanuni hizi, endapo utatokea mgogoro kati ya mmiliki wa leseni na mwezeshaji katika utekelezaji wa mkataba, mgogoro huo utatatuliwa kwa njia ya mazungumzo ya amani.

(2) Endapo pande zote zitashindwa kutatua mgogoro kwa njia ya mazungumzo ya amani, upande usioridhika

utawasilisha mgogoro huo kwenye vyombo vya kisheria vyenye mamlaka.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA JUMLA

Usimamizi na ufuatiliaji wa mikataba

**21.** Tume itakuwa na jukumu la kusimamia, kukagua, na kufuatilia utekelezaji wa mikataba yote ya misaada ya kiufundi.

Ukiukwaji

**22.** Mmiliki wa leseni ndogo ya uchimbaji madini anayekiuka masharti yaliyoainishwa chini ya Kanuni hizi atachukuliwa hatua kwa mujibu wa kifungu cha 63 cha Sheria.

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6(2))*

TAARIFA ZA UKAGUZI

**1. Hali ya Maendeleo ya Leseni**

Katika sehemu hii, taarifa itaainisha-

(a) jina la mmiliki na jina la mwezashaji, uraia na anuani yake, leseni, anuani na mahali leseni ilipo;

(b) idadi na namba za leseni zinazohusika kwa mkataba wa msaada wa kiufundi;

(c) tarehe ya kusainiwa kwa mkataba wa msaada wa kiufundi;

(d) shughuli za madini zilizotekelezwa katika eneo la leseni kuanzia tarehe ya kutolewa leseni;

(e) maendeleo yaliyofanyika katika eneo la leseni kulingana na matakwa ya Sheria;

(f) uhusiano uliopo kati ya mmiliki wa leseni na wachimbaji wengine wenye vitalu ndani ya eneo la leseni; na

(g) makubaliano yaliyofikiwa ya kufanya shughuli za madini kati ya mmiliki wa leseni na wachimbaji wadogo wenye maduara ndani ya eneo la leseni.

**2. Vibali au idhini iliyotolewa**

Katika sehemu hii, taarifa itaainisha-

(a) iwapo mpango wa utafutaji na uchimbaji wa madini umeandaliwa, umewasilishwa na au umeidhinishwa na Tume; na

(b) iwapo mpango wa usimamizi wa mazingira umeandaliwa, umewasilishwa na au umeidhinishwa na mamlaka husika.

**3. Urithishaji wa ujuzi na teknolojia kwa mmiliki wa leseni na wafanyakazi wake**

Katika sehemu hii, taarifa itaainisha-

(a) iwapo mpango wa urithishaji wa teknolojia, ujuzi na matumizi ya teknolojia kwa mmiliki wa leseni na wafanyakazi wake unatekelezeka; na

(b) iwapo mpango wa utaratibu wa kubadilishana maarifa na taarifa za msingi kuhusu teknolojia inayotumika kwenye uzalishaji na shughuli za utafiti wa madini unatekelezeka.

**4. Utekelezaji wa miradi ya wajibu wa wamiliki wa leseni kwa jamii|**

Sehemu hii itaainisha kuhusu mpango wa wajibu wa mmiliki wa leseni kwa jamii kulingana na matakwa ya Sheria na Kanuni za Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii.

**5. Changamoto zinazomkabili mmiliki wa leseni**

Katika sehemu hii, taarifa itaainisha-

(a) aina ya changamoto zinazomkabili mmiliki wa leseni; na

(b) hatua zilizochukuliwa kutatua changamoto hizo.

**6. Mapendekezo**

Katika sehemu hii, taarifa inapaswa kuainisha mapendekezo ya kitaalamu yatakayobainisha iwapo mmiliki wa leseni anastahili kupatiwa msaada wa kiufundi au la.

Dodoma,
17 Aprili, 2025

ANTHONY PETER MAVUNDE,
*Waziri wa Madini*

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA